Kutoka ***Mafatih ul Jinan***

SURA YA SITA

VITENDO VYA IBADA (AAMAL) KATIKA MWEZI WA DHUL HIJJA

Huu ni kati ya miezi yenye kuheshimiwa zaidi. Mwezi huu ulipoingia, vitendo vyema vya wafuasi wa mtume (masahaba) na wale wenye kumwogopa mwenyezi mungu vilidhihirika katika sala zao. Siku kumi za mwanzo za mwezi huu ni za muhimu sana kama zilivyonukuliwa katika kitabu Kitakatifu cha Mwenyezi Mungu cha Qur'an na zina baraka nyingi mno. Imeripotiwa kutoka kwa Mtume (s.a.w.w) kuwa vitendo vyema na ibada za sala zinazofanyika katika siku za kumi za kwanza za mwezi huu zinampendeza Mwenyezi Mungu zaidi kuliko zile zinazofanywa wakati mwingine wowote ule. Kuna vitendo kadhaa ambavyo vimependekezwa katika siku kumi hizi:

Kwanza: Kufunga kwa siku tisa za mwanzo za mwezi huu kuna natija sawa na aliyefunga kwa maisha yake yote.

Pili: Kusali rakaa mbili kila siku (katika nyusiku zinazotangulia siku kumi za mwanzo wa mwezi huu) baina ya sala ya Maghrib na Isha na katika kila rakaa, baada ya kusoma sura Al-Hamd na Ikhlas, soma aya ifuatayo mara moja:

(Arabic)

Mtu anayesali sala hizi malipo yake yanakuwa sawa na wale walioenda kufanya ibada ya Hijja.

Tatu: Kutoka mwanzo wa mwezi (wa Dhul Hijja) mpaka mchana wa siku ya Arafah, soma vifungu vya dua vifuatavyo baada ya sala za Fajr na kabla Maghrib. Imeripotiwa na Sheikh pamoja Seyyid kutoka Imam Ja'afar Sadiq (a.s):

(Arabic)

Nne: Soma vifungu vya dua hivi vitano kila siku vilivyoteremshwa na Jibril (a.s) kwa Hadhrat Issa (a.s) kama zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa siku kumi za mwanzo wa mwezi huu wa Dhul Hijja. Vifungu hivyo ni kama vifuatavyo:

(Arabic)

Hadhrat Issa (a.s) ameripotiwa kwamba ametaja juu ya natija kuu kwa kusoma vifungu hivi vitano mara mia moja. Allama Majlis amesema kwamba iwapo mtu atakisoma kila kifungu mara kumi kila siku, basi atakuwa amefuata mienendo ya Hadhrat Issa (a.s) lakini ni vyema kama vitasomwa mara mia moja.

Tano: Amiirul mu'uminiyn (a.s) ameripoti kuwa kusoma dua ifuatayo kila siku kwa siku kumi za mwanzo wa mwezi wa Dhul Hija kuna natija kubwa na vyema ikisomwa mara kumi:
(Arabic)

Aamal za ibada kwa siku maalum na siku / usiku unazozitangulia:

Siku ya kwanza

Ni siku takatifu sana na viko baadhi ya vitendo vya ibada ambavyo vinapendekezwa kufanywa mchana wa siku hii:

Kwanza: Kufunga siku hii kuna natija sawia na aliyefunga kwa miezi themanini (80)

Pili: Swala ya Fatima (a.s). Sheikh amenukuu kwamba swala hii ina Rakaa nne, sawia na swala ya Amiirul mu'uminin (a.s), katika kila rakaa baada ya kusoma sura ya Alhamdu, sura ya Ikhlas isomwe mara hamsini. Baada ya swala hiyo, tasbihi ya Hadhrat Fatima (a.s) isomwe halafu ifuatiwe na:

(Arabic)

Tatu: Swala ya Rakaa mbili iiswaliwe nusu saa kabla ya jua kufika utosini, na katika kila rakaa baada ya kusoma sura ya Alhamdu, mwenye kuswali asome kila mojawapo ya hizi mara kumi: sura ya Ikhlas, Ayatul Kursi na sura ya Qadr.

Nne: Yeyote ambaye anamwogopa mwenye kumnyanyasa (adui) wake asome kifungu kifuatacho:

(Arabic)

Mwenyezi Mungu atamwondolea masaibu yake ya kunyanyaswa.
Hadhrat Ibrahim (a.s) alizaliwa siku hii. Kulingana na Sheikh wawili, Hadhrat Fatima (a.s) aliolewa na Amiirul mu'uminin, Ali bin Abi Talib (a.s) siku hii pia.

Siku ya saba

Katika mwaka wa 114 A.H (hijiria) Imam Muhammad Baqir (a.s) aliuawa kishahidi siku hii katika mji wa Madina na ni siku ya huzuni kwa wafuasi wa dhehebu la kishia.

Siku ya nane.

Ni siku ya Tarwiya (kujaza maji kwa madhumuni ya kuyatumia wakati wa kusafiri). Kufunga katika siku hii kuna natija bora sana na imeripotiwa kwamba inakuwa kama kuomba msamaha kwa miaka sitini. Sheikh na Shaheed wamenukuu kwamba kuoga mwogo wa ghusl ni jambo linalopendekezwa kwa siku hii.

Siku / usiku unaotangulia siku ya tisa.

Ni usiku mtakatifu na wa ibada na dua. Katika usiku huu, msamaha, tauba na matakwa yako utakayomwomba Mwenyezi Mungu hukubaliwa. Ikiwa mtu atakesha kwa ibada katika usiku huu, Mwenyezi Mungu humtuza zawadi sawia na aliyeswali kwa miaka mia moja na sabini (170). Kuna baadhi ya aamal zinazopendekezwa katika usiku huu:

Kwanza: Soma dua ifuatayo kama vile ilivyoripotiwa kwamba atakayeisoma usiku huu (wa kutangulia siku ya tisa) ama usiku unaotangulia siku ya Ijumaa, atasamehewa:

(Arabic)

Pili: Soma mara elfu moja zile tasbih kumi zilizonukuliwa na Seyyid na ambazo zimo katika matendo ya ibada ya siku ya Arafah.

Tatu: Pia soma dua ya siku ya Arafah kama ilivyonukuliwa, na usiku wa siku ya Ijumaa, na imetengwa kuwa ni kati ya sehemu ya mwisho ya swala ya sita za usiku unaotangulia siku ya Ijumaa.

Nne: Zuru kaburi la Imam Husayn (a.s) huko Karbal na ubaki kuko huko hadi siku ya Eid ili uweze kuepushwa na madhara yoyote kwa mwaka huo.

Siku ya tisa

Ni siku ya Arafah na kati ya siku kuu zaidi, ijapo haijatajwa hivyo. Ni siku ambayo Mwenyezi Mungu huwaita viumbe Wake kuwa ni wenye kumwaabudu na kumtii Yeye. Neema na baraka Zake huwa kwa wingi na shetani hulaaniwa na kudhalilishwa. Imeripotiwa kuwa siku hii ya Arafah Imam Ali Zainul Abidiyn (a.s) alisikia sauti ya mwenye kuombaomba. Akamgekia huyo mtu mwenye kuombaomba na kumwambia "Hata huna haya wewe unayeombaomba asiyekuwa Mola wako siku hii?! Hata kwa mtoto aliye tumboni kwa mama yake, kuna matumaini kuwa neema ya Mwenyezi Mungu iko pamoja naye na atakuwa na matendo mema."
Katika siku hii kuna baadhi ya vitendo vya ibada ambavyo vimependekezwa:

Kwanza: Ghusl (mwogo / kuoga)

Pili: Ni ziyara ya Imam Husayn (a.s) ambayo ni sawa na kufanya ibada za faradhi elfu moja za hija na ibada elfu moja za sunna za hija, halkadhalika kupigana katika vita vitukufu elfu moja ama zaidi ya yote hayo. Kunamfululizo wa nukuu kuhusu ubora wa siku hii na mtu atakayekuwa na bahati ya kuwa chini ya paa la jengo mnamo kaburi la Imam Husayn (a.s) siku hii, mtu huyo anakuwa na hadhi na natija inayomshinda yule mtu aliyekatika jangwa la Arafah. Somo hili litajadiliwa zaidi katika kitengo cha sura ya ziyara (salam).

Tatu: Baada ya swala ya al asr na kabla ya kuanza kusoma dua za siku ya Arafah, swali rakaa mbili kwenye anga iliyowazi na ukubali madhambi yako uliyoyafanya kwa Mola wako ili yaweze kusamehewa na natija ya siku hiyo itapatikana. Baadaye unatakiwa uendelee kuswali na kuomba dua kama inavyopendekezwa kufanywa siku hii kulingana na nukuu za maimamu (a.s). Aamal nyingi sana zilizoripotiwa kufanywa, hivyo haingewezekana kunakili kila kitu hapa. Kafa'my amenukuu kwenye kitabu chake Misbah kwamba kufunga siku hii kumependekezwa kwa yule ambaye atakapofunga hatadhurika kiasi cha kutoweza kusoma dua na kwamba pia imependekezwa kufanya Ghusl na kusoma ziyara ya Imam Husayn (a.s) usiku inaotangulia siku ya Arafah na siku ya Arafah pia.
Wakati wa mchana, inatakiwa mtu aende kwenye uwanja katika anga iliyowazi na aswali sala za Dhuhr na Asr kwa umakini. Halafu swali rakaa mbili, ambapo baada ya kusoma sura Alhamdu, kwenye rakaa ya kwanza soma sura Ikhlas na katika rakaa ya pili soma sura Kaafiruun. Baadaye swali rakaa nne ambapo katika kila rakaa (kwa zile rakaa mbili za kwanza) baada ya kusoma sura alhamdu, soma sura Ikhlas mara hamsini. Hii ni swala ya Amirul mu'uminin (a.s) ambayo imejadiliwa kwenye sehemu ya matendo ya ibada kwa siku ya Ijumaa.
Halafu soma tasbih ifuatayo kama ilivyonukuliwa na Seyyid ibn Tawoos katika kitabu cha Iqbal kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w)

(Arabic)

Halafu soma kifungu (tasbih) kifuatacho mara mia moja:

(Arabic)

Halafu soma mara mia moja sura zifuatazo: sura Ikhlas, Ayatul Kursi na salawaat.
Soma vifungu vifuatavyo mara kumi kwa kila kimoja wapo.

(Arabic)

Na halafu usome haya yafuatayo:

(Arabic)

Halafu omba matakwa yako kuto kwa Mwenyezi Mungu na inshaallah, yatakubaliwa.
Soma salawaat ifuatayo, ambayo kulingana na Imam Ja'afar Sadiq (a.s) inamridhisha Mtukufu Mtume (s.a.w.w) na kizazi chake kitakatifu (a.s)

(Arabic)

Ile dua ya Ummi Dawood, ambayo imetengwa kama kitendo cha tano cha ibada katika siku ya tarehe 15 Rajab, pia ni sharti isomwe.
Baadaye soma tasbih ifuatayo ambayo ina natija zisizokadirika. Kutajwa kwa natija za tasbih hii kumeepukwa ili watu wawe na ushupavu na ni kama ifuatavyo hapa:

(Arabic)

Halafu sema:

(Arabic)

Halafu sema:

(Arabic)

Kisha sema:

(Arabic)

Kisha soma dua ambayo ni katika kitendo cha sita katika matendo ya ibada inayosomwa usiku unaofuatia siku ya Ijumaa.
Kisha soma dua ya imam Ali bin Husayn (a.s) iliyonukuliwa na Sheikh Toosi kwenye kitabu cha Misbah na inayoanza kama ifuatavyo:

(Arabic)

Dua hii ambayo inapaswa kusomwa kwenye jangwa la Arafah ni ndefu mno na haijaweza kunakiliwa yote hapa. Pia dua nambari 47 katika kitabu cha Sahifa Kamila, imependekezwa kusomwa kwa umakini mwingi na kwa hisia, kwa maana ina maombi ya kutoshelezewa matakwa ya kidunia na Akhera.